

## Kabla ya Ndoa:

\_\_\_\_\_ Je, umeidhinishwa kisheria kuendesha harusi kule Vermont?

- **Ikiwa wewe ni jaji au hakimu**, lazima uwe umekula kiapo rasmi cha kazi na lazima uendeshe harusi hiyo katika kipindi chako cha kazi.
- **Ikiwa umejiandikisha kwa Katibu wa Jimbo kama mfungisha ndoa wa muda**, utaidhinishwa kufungisha ndoa iliyobainishwa katika fomu ya kujiandikisha uliyowasilisha kwa Katibu wa Jimbo. Mamlaka yako ya kufungisha ndoa hiyo yataisha wakati sawa na wa leseni husika. Kwa maelezo kuhusu kujiandikisha kuwa mfungisha ndoa wa muda tembelea <https://sos.vermont.gov/> au upige simu kwa 802-828-2363.
- **Ikiwa wewe ni kasisi na unaishi Vermont**, lazima uwe umefanywa kasisi rasmi, umepewa leseni au kuidhinishwa na dhehebu lako.
- **Ikiwa wewe ni kasisi, lakini si mkaaji wa Vermont**, lazima upewe idhini maalum kutoka kwa mahakama ya kuthibitisha mirathi ya Vermont katika kaunti ambako utakuwa unafanyia sherehe, isipokuwa ikiwa unaishi katika jimbo au nchi inayopakana na kanisa lako, hekalu, msikiti au shirika lingine la kidini liloko Vermont au sehemu ya Vermont. Wasiliana na mahakama ya kuthibitisha mirathi kwa maelezo zaidi.

\_\_\_\_\_ Je, watu hawa wanastahiki kufunga ndoa kwa mujibu wa sheria ya Vermont?

\_\_\_\_\_ **Je, watu wote wawili wametia saina na kuandika tarehe katika sehemu za 15a-16b za Leseni na Cheti cha Ndoa ya Kiserikali cha Vermont**, na je, tarehe ya kufunga ndoa itakuwa ndani ya tarehe za "HALALI KUANZIA \_\_\_\_\_ HADI \_\_\_\_\_" zilizo kwenye leseni?

## Baada ya Ndoa:

\_\_\_\_\_ Jaza sehemu ya MFUNGISHA NDOA (18a-g) ukitumia taipureta au kuandika kwa **wino mweusi wa kudumu**.

MFUNGISHA NDOA	
Leseni hii inaidhinisha ndoa KULE VERMONT TU kwa wahusika waliotajwa hapo juu na mtu yeyote aliyeidhinishwa kisheria kufungisha ndoa.	
18a. NINATHIBITISHA KWAMBA WATU WALIO HAPO JUU WALIFUNGA NDOA MNAMO (Mwezi, Siku, Mwaka)	18b. MAHALI WALIKOFUNGA NDOA – JIJI AU MJI
18c. SAINI YA MTU ANAYETEKELEZA SHEREHE	18d. CHEO
18e. JINA (Charaza/Andika)	18f. NAMBARI YA SIMU
18g. ANWANI YA BARUA YA MTU ANAYETEKELEZA SHEREHE (Nambari na Mtaa, Jiji au Mji, Jimbo, Msimbo wa Eneo)	

- 18a.** Tarehe ya kufunga ndoa (inapendelewa kuandika jina la mwezi badala ya nambari (k.m. Julai 10, 2021, sio 7/10/21))
- 18b.** Jina la mji/jiji ambako sherehe ilifanyika (bainisha Jiji au Mji ikiwa inahitajika)
- 18c.** Saini yako
- 18e.** Jina lako lililoandikwa
- 18d.** Cheo chako (k.m. Mfungisha Ndoa wa Muda, Mchungaji, Padri, Rabi, Hakimu wa Amani, nk.)
- 18f.** Nambari yako bora zaidi ya mawasiliano ya simu
- 18g.** Anwani yako ya barua

\_\_\_\_\_ Ikiwa umeandikishwa na Katibu wa Jimbo kama mfungisha ndoa wa muda, nakala ya cheti cha idhini inapaswa kuambatishwa kwenye leseni iliyotiwa saina na kurejeshwa kwa karani wa mji aliyetoa leseni. (tazama 17c.)

\_\_\_\_\_ Sheria ya Vermont inahitaji cheti kilichojazwa kirejeshwe kwa karani wa mji aliyekupa **ndani ya siku 10** ili kuandikishwa. **Usikunje cheti hicho. Usiwapatie wanandoa cheti hicho.**